**FORM THREE HOLIDAY ASSIGNMENT FOR KISWAHILI**

**Swali la kwanza**

Tamthilia : Bembea ya Maisha ; Timothy Arege

Fafanua mabadiliko yanayojitokeza katika tamthilia ya Bembea ya maisha (alama20)

"Basi usijipandishe presha bure mama! "

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili

(alama4)

(b) Ainisha mbinu mbili za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili (alama2)

(c) Eleza sifa nne za msemewa (alama6)

(d) Jadili maudhui ya utamaduni kama yanavyojitokeza katika tamthilia mzima (alama10)

Mpambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine;

3. Jadili ufaafu wa anwani Mapambazuko ya Machweo (alama 20)

4. "Baba, wewe kila mara huhubiri mungu ni upendo. Mbona basi kumbagua"

a. Weka dondoo hili katika muktadha wake. (al.4)

b. Fafanua maudhui mawili katika dondoo hili (al.4)

c. Eleza umuhimu wa anayebaguliwa katika hadithi nzima. (al.12)

USHAIRI

SOMA SHAIRI HILI KISHA UJIBU MASWALI YANAYOFUATA

Ndege mwema na muruwa, katu haishi tunduni

Hataki kufadhiliwa, muda yumo utumwani

Japo mnyonyoe mbawa mwisho wake atahuni Ndege

kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa.

Ndege ataka yoyoma, nasiyahi msituni

Apite akisimama, shinani na mitawini

Haridhiki kwa mtama, na maji ya kikombeni

Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mwema wa hishima mwema mno wa kughani

Tundu huliona chama, japo liwe la thamani

Huporomosha yakwe kima, na kufanya faraghani

Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mpambe kwa zari, na lulu na marijani

Upambe yake suduri, kwa almasi kidani

Tunduni atahajiri, ili awe huriani

Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mwema wa busara, hatoishi kifungoni

Anayo kubwa hasara, kukosa nyumba ya mani

Lamkera lamkera, tundu la dhahabu kwani

Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege maumbile yake, na waja hayalingani

Yeye hutaka wenzake wafukuzane hewani

Jambo la kuishi mpweke, kamwe humridhiani

Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Baiti zangu ni haba, nakonea kituoni

Ndege huficha mahaba, kama yumo kifungoni

Hali ndege akashaba, kwani yumo adhabuni

Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

MASWALI

(a)Lipe shairi anwani mwafaka (alama 1)

(b)Fumbua maana ya ndege anayerejelewa (alama 1)

(c) Shairi hii ni la mkondo gani? (alama 3)

(d)Eleza muundo wa ubeti wa nne (alama 3)

(e) Fafanua uhuru aliotumia mshairi (alama 4)

(f) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (alama 4)

(g)Jadili dhamira ya mshairi (alama 2)

(h)Fafanua maana ya msamiati ufuatao kama ilivyotumiwa na mshairi

i) Atahuni

ii) Baiti

Soma shairi hili kasha ujibu maswali yanayofuatia

MKULIMA

Mtazameni ………nguzo ya Afrika Mtumwa wa

watumwa walioridhiya!

Amekita jembe lake akilisujudia

Kwa tambo liloumbuka na kuselehea

Uso ukifuka ukata ulojifanya tabia

Na machungu ya maonevu alovumilia

Moyo wako mzito ulokokomaa kama kuni

Haujui tena kutarajia wala kutamani

Unakufa ganzi, kutohisi raha wala huzuni

Basi iteni fikira mambo mukiyafikiri

Siku hamaki yake itapochafuka kama bahari

Siku ukweli wa hali yake utapodhihiri

Umejiandalia vipi…

Huo mkono ulomuumbua na kumkausha

Hizo pumzi zilomzimia taa ya maisha Kumfunga

kizuizi, gizani kumtowesha?

Ni jawabu gani alowekewa na wakati

Kuipoza ghadhabu ya kiu ingawa katiti

Kuiliwaza hamaki ya njaa hii ya dhati

Njaa ya maisha itakayo kushibishwa

MASWALI

(a) Eleza mambo muhimu yanayojitokeza katika shairi hili (alama 4)

(b) Taja na utoe mifano ya aina zozote mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili.

(c) Eleza maundo wa shairi hili (alama 3)

(d) Onyesha umuhimu wa matumizi ya kihisishi katika shairi (alama 2) (e) Fafanua maana ya:

(i) siku hamaki yake itapochafuka kama bahari (alama 2)

(ii) kuipoza ghadhabu ya kiy ingawa katiti (alama 2)

(f) Eleza maana ya msamiati ufuataokama ulivyotumiwa katika shairi

i) tambo

ii) ulokokomaa

iii) kumtowesha (alama 3)

FASIHI SIMULIZI

8. (I) Jamii ya waluo wana ohangla,

Waluhya wana Isukuti,

Wakikuyu wana mwomboko

Wakamba wana wathi na kilumi

Waswahili wana chakacha

(a) tambua kipera kina chorejelewa katika maelezo haya (alama 2)

(b) fafanua dhima ya kipera hiki (alama 8)

(ii) Eleza udhaifu wa mahojiano kama mbinu ya ukusanyanji wa data katika fasihi simulizi

(al 10)

**Swali la pili**

RIWAYA

NGUU ZA JADI

Anwani ya riwaya ya Nguu za Jadi ni ya kijazanda .Thibitisha kwa kurejelea riwaya nzima.

(alama 20)

TAMTHILIA

BEMBEA YA MAISHA

"Mwanangu usifanye hofu. Nikujuavyo mimi, hukuingia katika bahari si yako. Wala hakuna refu lisilokuwa na ncha. Yote yanakikomo eti. Ipo siku haya yote yatapita. Mkulima hodari ni libasi yake huwa imechakaa na kuchoka lakini moyoni anabaki safi kama theluji kwa kutosheka na tija ya sulubu zake. Huwezi kumlinganisha na mkulima wa nguo safi zilizopigwa pasi zikanyooka"

Chambua mtindo (alama10)

Jadili changamoto alizopitia msemewa wa maneno haya (alama10)

Eleza ufaafu wa anwani Bembea ya Maisha katika tamthilia ya Bembea ya Maisha (alama20)

HADITHI FUPI

MAPAMBAZUKO YA MACHWEO

Urumo umekita mzizi katika jumuiya ya Mapambazuko ya Machweo. Jadili (alama 20)

FADHILA ZA PUNDA

" Aligutuka kutoka kwenye usingizi wa mang'amung'amu, roho mkononi, pumzi zikimwenda mbio."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b) Mbona pumzi zilimwendea mbio na roho mkononi mrejelewa? (al.4)

c) Kwa kurejelea hadithi nzima, eleza madila anayopiyia mrejelewa. (al.12)

USHAIRI

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Alikwamba wako mama, kajifanya hupuliki,
Kakuasa kila jema, ukawa ng'oo! Hutaki,
Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,
Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,
Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindiki,
Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,
Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,
Mishikeli miania, kwako ona haitoki
Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,
Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo hadaa, kwa fukara na maliki,
Ulimwenguni shujaa, hilo kama hukumbuki,
Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,
Uliyataka mwenyew!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,
Ulijidhania samba, hutishiki na fataki,
Machangu yamekukumba, hata neno hutamki,
Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiriki,
Na tena ukajiona, kwamba we mstahiki,
Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,
Uliyataka mweyewe!

Maswali

a) Eleza dhamira ya shairi hili (al.2)

b) Tambua njia mbili anazotumia mtunzi wa shairi hili kuusisitiza ujumbe wake. (al.2)

c) Taja na utoe mifano ya aina zozote mbili za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi.

(al.4)

d) Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari/tutumbi (al.4)

e) Kwa kutoa mfano mmoja mmoja onyesha aina mbili za idhini ya kishairi katika shairi hili (al.4)

f)Bainisha toni ya shairi hili (al.2)

g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi (al.2)

i) mstahiki

ii) hupuliki

SHAIRI

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Nikiwa na njaa na matambara mwilini
Nimehudumika kama hayawani
Kupigwa na kutukanwa
Kimya kama kupita kwa shetani
Nafasi ya kupumzika hakuna
Ya kulala hakuna
Ya kuwaza hakuna
Basi kwani hili kufanyika
Ni kosa gani lilotendeka
Liloniletea adhabu hii isomalizika?
Ewe mwewe urukaye juu angani
Wajua lililomo mwangu moyoni
Niambie pale mipunga inapopepea
Ikatema miale ya jua
Mamangu bado angali amesimama akinisubiri?
Je nadhari hujitokeza usoni
Ikielekea huku kizuizini?
Mpenzi mama, nitarudi nyumbani
Nitarudi hata kama ni kifoni
Hata kama maiti yangu imekatikakatika
Vipande elfu, elfu kumi
Nitarudi nyumbani
Nikipenya kwenye ukuta huu

Nikipitia mwingine kama shetani

Nitarudi mpenzi mama...

Hata kama kifoni.

Maswali

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (al.1)

b) Tambua nafsineni katika shairi hili (al.2)

c) Eleza toni katika shairi hili (al.2)

d) Taja mambo manne ambayo mshairi analalamikia (al.4)

e) Fafanua dhamira katika shairi hili (al 2)

f)Thibitisha kuwa hili ni shairi huru (al 2)

g) Taja na ufafanue sifa mbili za mshairi (al 2)

h) Fafanua mbinu 3 za kimtindo zilizotumika katika ubeti wa tatu (al 3)

i)Eleza maana ya maneno yafuatoyo kama yalivyotumiwa katika shairi hili (al 2)

i) Hayawani

ii) Nadhari

FASIHI SIMULIZI

a) Maudhui na Fani ya maigizo hutegemea mwigizaji. Thibitisha kwa hoja tano. (al. 5)

b) Taja aina mbili za miviga (al. 2)

c) Eleza hasara tatu za miviga (al. 3)

d) Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

**Swali la Tatu**

TAMTHILIA

Bembea ya Maisha

Eleza ufaafu wa anwani Bembea ya Maisha katika tamthilia ya Bembea ya Maisha

USHAIRI

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Ewe hisia!

Umeniamshia ndoto niloisahau zamani

nyimbo ya kale

na mdundo usonivutia

ila hayawani na mwangu rohoni.

Tulia sasa tulia

Hebu tulia ewe hisia ulo mtimani

Nataka katu kusisimka

kwa sauti yako laini

Kwani njia zetu ni

daima hazioani

Umesubutu vipi kuniita

kutoka mwako ngomeni

ulimosahauliwa tangu zamani

Basi yawache maombolezi yako yaso maoni,

yawateke hao mashujaa wa kale

wafu walo kaburini.

Hebu tulia, usiniingilie

Usinihangaishe!

Kukuandama katu haimkini

Kwani hata sasa…kwa kukuwaza tu dakika hini

naona majuto ya mbali moyoni

kama kwamba nimegawa wangu wakati

na wazimu, majinuni.

Basi nenda zako hisia…shuu…hebu tokomea.

Maswali

(a) Huu ni utungo wa aina gani? (alama 2)

(b) Huku ukitoa mifano, fafanua sifa zinazoufanya utungo huu kuwa shairi (alama 5)

(c) Mistari mishata ni nini? Toa mifano kwenye shairi hili. (alama 4)

(d) Fafanua tamathali za kifasihi katika shairi hili. (alama 3)

(e) Eleza mbinu tatu alizotumia mtunzi kutosheleza kaida za kishairi. (alama 6)

Soma shairi lifwatalo kisha uyajibu maswali yanayoliandama:

Naandika yangu haya, kwa uwezo wa Wadudi,

Kanipa njema afiya, kumsifu sina budi,

Nifundishie insiya, hino methali ya jadi,

Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo

Ago mchama huuya, mbele mambo yakizidi,
Hurudi pakawa kaya, kupapenda hana budi,
Kwingi angawayawaya, ago shuruti arudi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Kule kwetu Mwarakaya, kijiji chetu cha jadi,
Yalidhihirika haya, bwana mmmoja mkaidi,
Aloalikwa ulaya, kadhani 'mepata sudi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo,

Alidhani hatauya, 'endapo nchi baidi,
Na kusema bila haya, kwa inda na ukaidi,
Kwamba akenda ulaya, harudi kwenya samadi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Aliranda akitaya, kwa mbwembwe na zake tadi,
Nguo moto kazitiya, nyumbaye akainadi,
Kasema vyote 'ishiya; kurudi sina ahadi
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Matusi aliyamwaya, mengi yasiyo idadi,
Mkewe kamwita yaya, na kudharau abidi,
Kanena 'mekata waya', ng'ambo nenda kufaidi,
Mchama ago hayeli, huenda akauya papo,

Ng'ambo alielekeya, kwa vishindo kama radi,
Kumbe aliyemwendeya, kabambwa kwa ufisadi,
Vya watu amebugiya, rushwa na kuhepa kodi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Kombo yakamwendeya, mambo mno yakazidi,
Akababakia kuliya, nyumbani ataka rudi,
Nyumba ipi 'taingiya', hana tena tabaradi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo

Maswali

a) Kwa kutolea ushahidi ufaao shairini, jadili kifupi maswala matatu makuu ambayo mtunzi ameyashughulikia. (alama 6)

b) “Mtunzi huyu ni bingwa wa kutumia lugha kupitisha ujumbe.” Tetea. (alama 4)

c) Fasiri ujumbe wa mtunzi katika ubeti wa sita. (alama 4)

d)Nafsi nenewa katika shairi hili ni nani? Thibitisha. (alama 2)

e) Zaidi ya tarbia, ungelipangaje tena shairi hili? (alama 2)

f) Fafanua msamiati ufwatao kama ulivyotumika shairini: (alama 2)

i. Baidi

ii. ‘mekata waya’

HADITHI FUPI

Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine

Rachel Wangari katika hadithi ya mapambazuko ametumia mbinu ya JAZANDA kwa upana.

Jadili alama 20

" Hawajui hawa....Haitoshi yeyote yule kulijaza pengo aliloliacha mke wangu mpenzi."

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b. Fafanua maudhui matatu yanayojitokeza katika dondoo hili. (al.6)

c. Fafanua nafasi ya aliyeacha pengo katika kujenga maudhui hadithi ni. (al.10)

FASIHI SIMULIZI

“Magwiji wa uwanda mpana wa tamaduni za Kiafrika: wazee walioila chumvi wakabobea katika falsafa za turathi zetu, maghuluma wenye misuli tinginya na vifua vya mfumbata vinavyostahimili hujuma za kila nui na malaika wa kike uliosheheni mizinga na chemichemi ya urembo, nawasabahi. Wa zamani waliamba kuwa mwacha mila ni mtuma. Turathi zetu ni uhai. Turathi zetu ni msingi wa ubinadamu wetu. Turathi zetu zinabeba mustakabali wetu. Tuzienzi kama tuenzivyo asali.”

Maswali

(a) (i)Tambua kipera cha utanzu wa mazungumzo kinachohusishwa na kifungu hiki. (alama 1)

(ii)Thibitisha jibu lako katika (i) kwa mifano yoyote mitatu. (alama 3)

(b)Iwapo umehudhuria utendaji wa kipera hiki nyanjani eleza sifa tano za mtendaji utakazoziona zisizojitokeza kwenye kifungu. (alama 5)

(c)Taja na kueleza miktadha minne ambamo kipera hiki kinaweza kutumiwa katika jamii ya kisasa. (alama 4)

(d) Andika sifa zozote nne za jamii ya nafsi neni katika utungo huu. (alama 4 )

(e) Eleza njia tatu za ukusanyaji wa data unazoweza kutumia kukusanya data kuhusu kipera hiki.

(alama 3)

RIWAYA

Clara Momanyi: Nguu za Jadi

"Alitazama jinsi kina mama wengine walijikunyata na kutokana na kibaridi kile cha asubuhi"

a. Elea muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b. Tambua mbinu ya lugha katika dondoo hili. (al.2)

c. Fafanua umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (al.14)

Eleza jinsi Chifu Mshabaha amekuza dhana zifuatazo riwayani.

a) Unafiki

b) Ufisadi

c) Udhalimu/katili

Kwa kurejelea riwaya nzima, thibitisha kuwa Chifu Mshabaha ni mwenye Madharau. (al.10)